Imefadhiliwa na
Umoja wa Ulaya

# CODE-P Mradi wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Kahawa Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania

**CODE-P inachangia katika maendeleo shirikishi na endelevu ya mnyororo wa thamani wa kahawa katika mikoa ya Ruvuma, Mbeya, na Songwe nchini Tanzania**



## TAARIFA MUHIMU

**Sekta:** Kilimo (Kahawa)
**Mshirika Kiongozi:** Vi Agroforestry
**Washirika Wengine:** Jukwaa la wadau wa Kilimo Wasio wa Kiserikali (ANSAF), BRAC International, Café Africa Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI)
**Bajeti:** EUR 3 750 000
**Mchango wa EU:** EUR 3 000 000
**Muda wa Mradi:** 2020 - 2024

## USULI





Ijapokuwa Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania zina hali nzuri ya hewa na mazingira mengine mazuri kwa ajili ya kilimo cha kahawa, wastani wa uzalishaji wa kahawa ndani ya miaka mitano iliyopita katika mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma umekuwa chini sana katika kiwango cha kilo 0.54 tu kwa kila mti (tani 0.748 kwa hekta), ikilinganishwa na kilo 1.8 kwa kila mti katika mikoa ya Magharibi mwa Tanzania.

Changamoto kubwa ambazo zinahitajika kukabiliwa kupitia CODE-P ni pamoja na tija ndogo na uzalishaji mdogo wa kahawa bora, upungufu katika huduma za ugani, bei kubwa na ufikiaji mdogo wa pembejeo za kilimo zinazoaminika. Sababu zingine ni pamoja na mbinu duni za sayansi ya uchumi wa kilimo, kuyumba kwa bei ya kahawa sokoni, ukosefu wa taasisi za kifedha zinazowekeza katika mnyororo wa thamani wa kahawa, na faida ndogo au kutokwepo kwa faida kabisa katika mauzo ya kahawa kwa wanawake na vijana. Haya yote yanachangia kusababisha uzalishaji mdogo, na kuwaacha wakulima katika umaskini.

Mpango wa utekelezaji wa CODE-P umeandaliwa kutokana na msingi huu na unalenga kufanikisha maendeleo ya maeneo ya sekta ndogo ya kahawa katika Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania.

**AGRI-CONNECT**

Kusaidia Minyororo ya Thamani kwa Ustawi wa Pamoja katika Mazao ya Kahawa, Chai na Bustani

## MAELEZO YA MRADI

Ili kufikia lengo kuu la CODE-P, mikakati ifuatayo itatumiwa:

- Kuendeleza na kuimarisha vyama vya ushirika vya kahawa vidogo kama nyenzo muhimu ya utoaji wa huduma za msaada ambazo zinawezesha uzalishaji, usindikaji na biashara ya kahawa inayozalishwa na wakulima wadogo.
- Kuhamasisha ukuaji wa uchumi unaoongozwa na biashara katika Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania.

Mikakati hii itafikiwa kupitia:

- Kuimarisha ushindani wa wazalishaji wadogo wa kahawa.
- Kukuza uwekezaji wa sekta binafsi na utengenezaji wa ajira katika mnyororo wa thamani wa kahawa.
- Kuboresha usalama wa chakula na lishe katika mikoa husika.
-

Hizi ndizo baadhi ya shughuli muhimu za CODE-P:

- Kukuza upitishwaji wa mbinu za Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Kilimo.
- Kuwezesha uzidishwaji na usambazaji wa miche milioni 7 ya kahawa kwa wakulima.
- Kuongeza uwezo wa wakulima wadogo na vyama vya ushirika kuhusiana na mbinu ya usimamizi wa mazao baada ya mavuno.
- Kukuza upatikanaji, ufikiaji, na mahusiano na taasisi za kifedha.
- Kuwezesha uhusiano wa kimasoko na matumizi ya majukwaa ya dijitali kwa ajili ya kupata habari za soko.
- Kampeni zinazolenga lishe.
- Kukuza mazungumzo kati ya wahusika katika mnyororo wa thamani wa kahawa.
- Kufanya utetezi unaotegemea uthibitisho wa sera ya mazingira inayozuia ukuzaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa.

## MATOKEO YATARAJIWAYO

Mradi unatarajia:

- Kufikia wakulima wadogo 24,000 (wasichana 14,400 na vijana 9,600 wenye umri kati ya miaka 18-35) na kuwapa ujuzi wa uzalishaji, uvunaji, uuzaji, pamoja na uelewa kuhusu masuala ya kifedha.
- Kuimarisha vyama vya ushirika 60 vya msingi vya kahawa vinavyofanya kazi katika maeneo yaliyolengwa na kukarabati mashine za kumenyea kahawa 60 ili zigeuzwe kuwa vituo vya kutoa na kusambaza pembejeo za kilimo, teknolojia, na habari.
- Kusaidia maafisa ugani wa serikali na wadau wengine wanaohusika na sera na mipango katika ngazi ya mtaa/kijiji kupata mafunzo ya mbinu za usimamizi endelevu wa ardhi ya kilimo na mbinu zingine endelevu za kilimo cha kahawa.
- Kusaidia wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa kahawa kushirikiana kuboresha utendaji wa sekta ndogo ya kahawa.

Ifikapo mwisho wa mradi, matokeo makuu matatu yanatarajiwa kupatikana:

- Kuongezeka kwa uzalishaji unaohimili mbadailiko ya tabianchi na wa kahawa bora.
- Kuongezeka kwa mapato kutokana na usimamizi wa mazao baada ya mavuno ulioboreshwa, kwa uwezo wa usindikaji na uhusiano wa kimasoko (kati ya wakulima wadogo, wanawake na wanaume, biashara ndogo na za kati) na huduma za kifedha.
- Kuimarishwa kwa ushindani wa mnyororo wa thamani wa kahawa wenye mfumo wa sera na udhibiti ulio na manufaa.

## WASHIRIKI

Vi Agroforestry · TaCRI Tanzania Coffee Research Institute · Café Africa · brac · ANSAF Agricultural Non State Actors Forum

## MAWASILIANO


**Vi Agroforestry/Vi-skogen (Country Office)**
Plot 44, Mtaa wa Uporoto, S.L.P 7157, Dar Es Salaam, Tanzania
Barua Pepe: tanzania@viagroforestry.org | Tovuti: www.viagroforestry.org

**Ofisi za Mradi:**
Mbozi: TACRI Mbimba Station, Brac Maendeleo; Mbeya: Café Africa in Mwalimu House building
Mbinga: TACRI Ugano Station, Brac Maendeleo



Imefadhiliwa na Umoja wa Ulaya



Email: delegation-tanzania@eeas.europa.eu
https://www.eeas.europa.eu/delegations/tanzania

EuropeanUnionTanzania
EUinTZ